## VIGEZO NA MASHARTI

1. SUPA FAN ni shindano lenye raundi tatu linalowazawadia mashabiki watatu safari iliyolipiwa na benki ya CRDB kusafiri na timu wanayoshabikia ambayo itachukua ubingwa wa CRDB Bank Federation Cup msimu wa 2024/25. Safari hiyo itakuwa ni ya mechi ya kwanza ya ugenini baada ya Shirikisho la Soka barani Afrika CAF kupanga droo ya mashindano ya Ligi ya mabingwa Afrika au Kombe la Shirikisho Afrika msimu wa 2025/2026.

2. Shindano litaanza Juni 20 na kumalizika Julai 13 likigawanyika kwenye raundi tatu.

3. Raundi ya kwanza ya shindano itafanyika kwenye kurasa za Instagram za @crdbbanksports na @crdbbankplc ambapo kila siku kwa siku 10 mfululizo litaulizwa swali moja huku kila mshiriki akitakiwa kuweka jibu sahihi kwenye sehemu ya comment likiambatana na timu anayoshabikia kati ya timu mbili zitakazokuwa zimeingia fainali ya CRDB Bank Federation Cup. Watu 20 wa kwanza kujibu kwa usahihi wataingia kwenye raundi ya pili. Katika raundi hii ya kwanza, jumla ya washindi 200 watapatikana.

4. Washindi 20 wa kila swali hawataruhusiwa kushiriki kwenye swali linalofuata, na endapo watashiriki tena basi hawatachaguliwa ili kuwapa nafasi washiriki wengine.

5. Raundi ya pili itahusisha washindi 200 kutoka Instagram ambao watatakiwa kufanya miamala kupitia SimBanking App au USSD ya *150*03# ili kujiongezea nafasi ya kuingia kwenye raundi ya tatu. Mashabiki wa timu itakayofungwa kwenye mchezo wa fainali wataondolewa kwenye shindano na kubaki na wale ambao timu yao itachukua ubingwa.

6. Baada ya mchezo wa fainali, mashabiki wa timu itakayoibuka bingwa wa CRDB Bank Federation Cup msimu wa 2024/25 wataingia raundi ya tatu ambapo watapewa wiki moja zaidi ya kufanya miamala ya SimBanking. Mashabiki 10 kati yao wenye miamala mingi zaidi wataingia kwenye droo ya mwisho ya kupata washindi wa jumla watatu ambayo itafanyika na kuonyeshwa Live Azam TV ambao ni washirika wetu katika CRDB Bank Federation Cup wakiwa ndio warusha matangazo pekee.

7. Washindi watalipiwa tiketi ya ndege, malazi, usafiri wa ndani wakiwa nchi ya ugenini, nafasi ya kuhudhuria mazoezi ya mwisho ya timu yao siku moja kabla ya mechi, kupiga picha na wachezaji wa timu yao baada ya mazoezi, tiketi za kuingilia kwenye mechi pamoja na pesa ya kujikimu (Tsh 1,000,000/=) kila mmoja.

8. Ili kushinda, mshiriki anatakiwa ku-follow kurasa za Instagram za @crdbbankplc na @crdbbanksports, kucomment jibu sahihi la swali na timu anayoshabikia.

Classification: CRDB Internal

9. Mshiriki pia anatakiwa kuwa na akaunti ya CRDB na anafanya miamala yake kwa SimBanking App au *150*03#.

10. Mshiriki anatakiwa kuwa raia wa Tanzania mwenye pasi ya kusafiria.